TOLEO NO.64

# Khilafah

(MUHARAMU 1447 HIJIRIA —JULAI 2025 MILADIA) ( Bei Tsh 4,000/= - Ksh 200/=)

NDIO SULUHISHO

## NI DHAMBI KUBWA KWA NDEGE ZA MAYAHUDI KUVUKA ANGA YATAWALA, KUIPIGA MABOMU IRAN NA KURUDI SALAMA BILA KUTUN-



**Trump alisema katika chapisho kwenye jukwaa la Kijamii la 'Truth'**: ["Iran na Israel wanapaswa kufanya makubaliano, na watafanya makubaliano, kama vile nilivyozifanya India na Pakistan kufanya." Aliendelea: "Vivyo hivyo, tutakuwa na AMANI, hivi karibuni, kati ya Israel na Iran! Miito mingi na mikutano inafanyika hivi sasa."(Sky News,15/6/2025). Mnamo Jumapili, msemaji wa jeshi la umbile la Kiyahudi alisema kupitia jukwaa la X kwamba "Israel ilitoa onyo kwa Wairan wanaoishi karibu na vinu vya nyuklia nchini Iran kuhama makaazi yao." Wakati huo msemaji wa jeshi la 'Israel' alisema kuwa jeshi lilishambulia kituo cha nyuklia katika mji wa Isfahan, katikati mwa Iran. Tangu alfajiri ya Jumapili, Iran ilianza kurusha raundi mpya za makombora kwenye shabaha ndani ya 'Israel', na kusababisha vifo na makumi ya majeruhi, na kusababisha uharibifu mkubwa kwa nyumba na majengo. Kwa kujibu, Tehran imekuwa chini ya mashambulizi ya 'Israeli'. (Al Jazeera,15/6/2025).

**Inaendelea Uk. 3**

## BAJETI YA TANZANIA 2025 INAAKISI UFUJAJI WA MALI




Alkhamisi Juni 12, 2025 Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba aliwasilisha bajeti kuu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/26 bungeni jijini Dodoma. Katika bajeti hiyo, serikali imeweka vipaumbele kadhaa vinavyoakisi kwa jinsi gani serikali za kidemokrasia zisivyomjali raia masikini wa kawaida kwa kuwekeza katika matumizi yasiyo ya lazima. Vipaumbele vya serikali havigusi kutatua masuala ya msingi ya mwananchi.

Bajeti hii ya Serikali kwa mwaka huu wa Fedha 2025/2026 inakadiriwa kuwa ni shilingi trilioni 56.49 zitakazotumika kwa kiasi kikubwa katika kugharamia deni la serikali, ujenzi na ukarabati wa viwanja vya michezo kwa ajili ya maandalizi ya michuano **Uk. 6**



## Yaliyomo :


- **Mwaka Mpya Wa Kiislamu Utupe Msukumo Mpya…………...2**
- **Kiinua Mgongo Mwisho Wa Utumishi ………………………….4**
- **Vita Ya Irani na Israel hatari zake kwa ummah ……….……....5**
- **Kampeni Maalum ya Kulinda na kutetea Aqida ya Kiislamu...8**

# MWAKA MPYA WA KIISLAMU UTUPE MSUKUMO MPYA

Mwaka mpya wa Kiislamu wa 1447 Hijria umeingia, jarida la Khilafah linachukua fursa hii kuupongeza Umma wote wa Kiislamu kwa kuingia mwaka huo.

Kuanza kwa mwaka mwengine kuna maana kadhaa ambazo Umma wa Kiislamu unafaa kuzingatia kwa makini sana ikiambatana na kuchukua hatua za kivitendo.

Kujiri mwaka mpya humaanisha kuongezeka kwa umri wetu na kuwa karibu zaidi na kaburi kuelekea kwa Mola wetu, yaani akhera. Jambo hili litusukume kujifunga na Uislamu wetu kwa kufanya tuliyoamrishwa na kuacha yaliokatazwa, na huko ndio maana ya kufanya matayarisho ya mauti ambayo huja ghafla bila ya taarifa. Maandalizi ya mauti au safari ya akhera ndio moja katika maana ya taqwa kwa mujibu wa Imamu Ally ra. alipotoa ufafanuzi wa dhana ya taqwa.

Aidha, kuingia mwaka mpya, kwa kuwa leo hatuna dola ya Kiislamu (Khilafah) maana yake tumeingia katika mwaka mwengine wa madhila, mashaka na maumivu kwa Umma wetu wote. Kwa sababu tangu kuangushwa dola yetu tukufu ya Khilafah Uthmania mwaka 1342 Hijria/ 1924 Miladia Umma wetu haujawahi tena kupita siku bila ya kusibiwa na maumivu, mashaka , dhulma, mauaji kutoka kwa makafiri au wakala wao, kwa kuwa ngao yetu ( Khilafah ) haipo tena.

Kwa hivyo, kuanza mwaka huu mpya wa 1447 maana yake tumeshaishi katika hali ya dhulma na idhilali ya makafiri kwa miaka 105 tangu kuangushwa Khilafah mwaka 1342 Hijria/ 1924 Miladia.

Hali hii itupe ghera na msukumo zaidi na zaidi wa kufanya kazi ya kulingania Uislamu ili tufikie ukombozi wa Umma wetu wote.

Na zingatio la mwisho kufuatia kuingia mwaka mpya ni jambo nyeti tunapalopaswa kulikumbuka kwamba kalenda hii ya Hijria iliasisiwa rasmi wakati wa Khilafah ya Umar bin Khatab katika mwaka wa 16AH.

Baada ya mashauriano na makubaliano na masahaba wakubwa (ijmaa), ambapo wakakubaliana tukio kubwa la 'Hijra' ndio liwe nukta kianzio cha mwaka wa kuihesabu kalenda hiyo.

Uchaguzi wa tukio la 'Hijra'ulifikiwa kwa msimamo mmoja licha ya kuwepo matukio mengine makubwa katika tareekh ya Kiislamu kama vile Uzawa wa Mtume SAAW, kupewa Utume, Safari ya Israi na Miiraj, Kufariki kwake nk.

Matukio yote hayo yakiwa makubwa yaliachwa si kwa kuwa si muhimu, lakini likachaguliwa na kuchukuliwa tukio tukufu la 'Hijra' kwa kuwa ndilo lililochora mstari muhimu wa maisha ya Waislamu kutoka kuwa chini ya utawala wa kikafiri ndani ya Makka na kuanza maisha mapya ya kutawaliwa na dola yao tukufu ya mwanzo ya Kiislamu ndani ya Madina.

Hijra ni tukio la safari aliyoifanya Mtume (S.A.A.W) kutoka Makka kuelekea Madina akiwa tayari ametawazwa kuwa kiongozi rasmi wa dola ya mwanzo ya Kiislamu.

Kwa hivyo, uchaguzi wa masahaba wa tukio la Hijra kama nukta kianzio cha kalenda yetu maana yake wanatukumbusha mpaka Siku ya Kiama ulazima na uwajibu wa kuwa chini ya kivuli cha dola moja ya Kiislamu ( Khilafah).

Ikiwa ni hivyo, wakati tukiwapongeaz Umma wetu kwa kuanza mwaka mpya wa 1447 Hijria na tukimuomba Allah Taala Ajaalie uwe mwaka wa kupata nusra na kurejea izza yetu, pia tuwakumbusha Waislamu uwajibu mkubwa juu ya shingo zao wa kulingania au kuungana na wanaolingania kurejeshwa tena dola ya Kiislamu ili kuusimamia Uislamu na Waislamu kama tukio la Hijra linavyotuonesha.

1 **MUHARRAM1447**

**JUNI 2025 MILADI**

**MHARIRI ……..**

**USIKOSE KUSOMA JARIDA LAKO LA KHILAFAH KILA MWEZI**

## Ni Dhambi Kubwa Kwa Ndege Za Mayahudi ...

*Kutoka uk .1*

**Umbile la Kiyahudi lilitangaza mnamo Jumamosi, 14/6/2025**, kwamba wanasayansi 9 na wataalamu katika mpango wa nyuklia wa Iran waliuawa wakati wa uvamizi wake nchini, na hivyo kuongeza idadi ya vifo iliyotangazwa hapo awali, nao ni: Ali Bakhoy Karimi, Mansour Askari, na Saeed Borji, ambao ni wataalamu wa mekaniki, fizikia, na vifaa vya uhandisi, mtawaliwa, katika uvamizi mnamo Ijumaa, kwa mujibu wa jeshi. Hili lilikuja katika tangazo lililothibitishwa na Shirika la Habari la Tasnim la Iran. Umbile la Kiyahudi lilikuwa limeanzisha "shambulizi ambalo halijawahi kushuhudiwa nchini Iran alfajiri ya Ijumaa, 13/6/2025, likilenga kitovu cha mpango wa nyuklia wa Iran na viongozi wakuu wa kijeshi. Huku Iran ikithibitisha kwamba ilirusha mamia ya makombora mnamo Ijumaa jioni mwanzoni mwa jibu lake kwa Israel." (CNN, 14/6/2025)

**Mara tu baada ya shambulizi la Kiyahudi, Rais wa Marekani Donald Trump alitangaza mnamo Ijumaa, 13/6/2025:** [“Shambulizi la Israel dhidi ya Iran limekuwa bora kabisa,” akiitaka ikamilishe makubaliano kuhusu mpango wake wa nyuklia. Akijibu swali kutoka kwa ABC: "Je, kuna dori ya Marekani katika shambulizi la Iran?" alisema, “Sitaki kujibu hilo.” Alisema kwenye jukwaa la Kijamii la ‘Truth’, "Iran lazima ifanye mapatano, kabla haijapoteza kila kitu, na kuokoa kile ambacho hapo awali kilijulikana kama Himaya ya Iran." Aliongeza kuwa aliionya Tehran kwamba "Marekani inatengeneza zana bora zaidi za kijeshi zenye hatari zaidi popote duniani ... Israel inazo nyingi, na nyingi zaidi zinakuja - na wanajua jinsi ya kuzitumia." Katika taarifa mithili ya hizo, Trump alisema: "Leo ni siku ya 61. Niliwaambia la kufanya, lakini hawakuweza kufika huko. Sasa wamefika, labda, ni nafasi ya pili!" (Al Jazeera, 13/6/2025)]

**Kwa kutafakari matukio haya, yafuatayo yanadhihirika:**

1- Ni wazi kutokana na matukio haya kwamba Mayahudi hawakuishambulia Iran isipokuwa kwa amri ya Marekani ya Trump, kwani kauli zake zinaeleza haya kwa uwazi. Hili ni hakika na linatarajiwa, kwa kuwa Mayahudi hawana uwezo wao wenyewe, wala hawana uwezo wa kupigana. Mwenyezi Mungu Mtukufu, Aliyetukuka, ni Mkweli zaidi:

**[ لَنْ يَضُرُّوكُمْ إِلَّا أَذًى وَإِنْ يُقَاتِلُوكُمْ يُوَلُّوكُمُ الْأَدْبَارَ ثُمَّ لَا يُنْصَرُونَ * ضُرِبَتْ عَلَيْهِمُ الذِّلَّةُ أَيْنَ مَا ثُقِفُوا إِلَّا بِحَبْلٍ مِنَ اللَّهِ وَحَبْلٍ مِنَ النَّاسِ وَبَاءُوا بِغَضَبٍ مِنَ اللَّهِ وَضُرِبَتْ عَلَيْهِمُ الْمَسْكَنَةُ]**

**“Maadui hawatakudhuruni ila ni maudhi tu. Na wakipigana nanyi watakupeni mgongo, na tena hawatanusuriwa. * Wamepigwa na udhalili popote wanapo kutikana, isipo kuwa wakishika kamba ya Mwenyezi Mungu na kamba ya watu. Na wakastahiki ghadhabu ya Mwenyezi Mungu, na wamepigwa na unyonge.”** [Aal-i-Imran: 111-2]. Hivyo, tangu zama zao za mwanzo, wameikata kamba ya Mwenyezi Mungu baada ya zama za Mitume wao. Na ni vivyo hivyo katika zama za kisasa, kama vile Uingereza iliwatabanni tangu Vita vya Kwanza vya Dunia, kisha wakahamia kukumbatia Amerika baada ya Vita vya Pili vya Dunia. Vita vyao vyote vinazungumza juu ya hilo, kwa kuwa wako kwenye kamba ya watu… Usaidizi wa Trump kwao katika shambulizi lao dhidi ya Iran uko wazi kutokana na kauli za Trump hapo juu kwa yeyote aliye na moyo au anayesikiliza kwa makini.

2- Kisha lililo kubwa zaidi kuliko hili na la maafa na machungu zaidi ni kwamba ndege za Mayahudi zilivuka anga za tawala zinazotawala katika nchi za Kiislamu zinazozunguka umbile la Kiyahudi, ambazo ziliharibu na kuua huku zikiwa Iran na kisha zikaregea katika ardhi inayokaliwa kwa mabavu kwa usalama na amani. Hakuna hata risasi moja iliyorushwa kwa ndege hizi na watawala waliowazunguka huko Ash-Sham, Iraq, Misri, Uturuki na kutoka kila mahali… Hivyo, wanavuka mipaka na kushambulia wakiwa salama, wakienda na kurudi, na watawala katika nchi za Kiislamu wakitazama yale yaliyokuwa yakitendeka bila kuchukua hatua. Walisahau au kujifanya kusahau matokeo ya uhalifu wa kimya chao.

**[ سَيُصِيبُ الَّذِينَ أَجْرَمُوا صَغَارٌ عِنْدَ اللَّهِ وَعَذَابٌ شَدِيدٌ بِمَا كَانُوا يَمْكُرُونَ]**

**“Itawafikia hao walio kosa udhalili na adhabu kali kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu ya vitimbi walivyo kuwa wakivifanya.”** [Al-An’am: 124]. Ni dhambi kubwa kwamba ndege za Kiyahudi huvuka anga ya watawala vibaraka,

**Inaendelea Uk. 7**

## KIINUA MGONGO MWISHO WA UTUMISHI

**Swali:**

Asalaam alaykum,

Ni ipi hukmu ya kisharia ya kuchukua kiinua mgongo mwisho wa utumishi kwa ajili ya mfayanyakazi aliyetumia miaka kadhaa katika kazi yake kwa uzuri na akadai mshahara wake "waliowafikiana" kutoka kwa mwenye kazi bila ya dhulma au kasoro katika kipindi chote cha kazi yake?

Kwa maelezo mengine, je huzingatiwa kiinua mgongo mwisho wa utumishi kulikotajwa katika kanuni iliyopo na inayofanyiwa kazi leo ni haki ya kisharia kwa ajili ya mfanyakazi aliyemaliza muda wake wa kazi? Na je huzingatiwa yule mwenye kazi kukataa kulipa fedha za malipo ya kiinua mgongo ni kula haki (ya mwengine) na kutenda haramu?

Huku tukizingatia kwamba kanuni iliyopo inaeleza kwamba theluthi moja ya kiwango cha mshahara wake wa kila mwezi kwa kila mwaka wa utumishi alipwe mfayakazi aliyetumikia katika kazi yake kwa muda wa chini ya miaka 5, na theluthi mbili ya mshahara kwa kila mwaka wa utumishi kwa mfanyakazi aliyetumikia katika kazi yake kuanzia miaka 5 – 10, na mshahara kamili kwa mwenye kuvuka miaka 10 katika utumishi.

**Jawabu:**

Waalaykum Salam Warahmatullah Wabarakatuh,

Ewe ndugu yetu Hakika Waislamu hupaswa kufuata masharti yao( waliyowekeana)



kama ilivyoelezwa katika Hadithi tukufu, ambayo ameitoa Tirmidh katika *Sunan* yake na akielezea kuwa ni Hadithi *hasan* na ni sahihi:

"Ametueleza Kathir bin Abdillah bin Amr bin Auf Al-Muzani kutoka kwa baba yake kutoka kwa babu yake kwamba Mtume (SAAW) amesema:

***"Na Waislamu wanalazimika kufata masharti yao (waliyowekeana) isipokua sharti lililoharamisha halali au lililohalalisha haramu".***

Hivyo basi, ikiwa pameelezwa katika mkataba wa kazi kati ya mfanyakazi na mwenye kazi sharti kwamba mfanyakazi atalipwa kiinua mgongo fulani mwisho wa utumishi, basi itakua ni haki ya mfanyakzi kwa mujibu wa sharti la mkataba.

Vilevile, ikiwa mkataba wa kazi kati ya mfanyakazi na mwenye kazi unafuata kanuni ya masharti ya kanuni ya kazi inayotakiwa kutendwa na mwenye kazi, na ikawa kanuni hii inaeleza kwamba mfanyakazi atalipwa kiinua mgongo fulani mwisho wa utumishi, basi kitakua (kiinua mgongo hicho) ni haki ya mfanyakazi kwa mujibu wa sharti la mkataba.

Ikiwa hakuna lolote lililotajwa katika haya kama ilivyobainishwa hapo juu, basi hupewa mshahara wake tu (huyo mfanyakazi) na hatalipwa kiinua mgongo cha mwisho wa utumishi.

Haya ndiyo ninayoyaona sawa katika mas-ala haya. Na nataraji yamekaa wazi, na Allah ndie Muzi zaidi na Mwenye hekima zaidi.

Ndugu yenu Ata ibn Khalil Abu Rashta

Amiri wa Hizb ut Tahrir

11, Rajab 1440H

13, March 2019.

## Ni Dhambi... *Kutoka uk .3*

kutekeleza mashambulizi yao na kurudi bila ya kutunguliwa na yeyote kati ya watawala hao.

3- Kila mwenye akili timamu anatambua kuwa njia bora ya kujilinda dhidi ya Mayahudi ni mashambulizi. Mayahudi wamekuwa wakitishia Iran kwa muda mrefu, haswa katika siku za hivi karibuni. Trump hata alidokeza na hata kutangaza kwamba Mayahudi watashambulia vituo vya nyuklia vya Iran. Hata hivyo, Iran haikuanzisha jibu la mashambulizi dhidi ya Mayahudi, katika kuilinda Iran, na kuepusha vitisho hivi kutoka kwa Marekani na Mayahudi. Hii inashangaza kwa kweli!! Iran ilikaa kimya hadi mitambo yake iliposhambuliwa na wanasayansi wake kuuawa, na ndipo ikaanza kujibu. Licha ya mashambulizi yote mfululizo, Trump anaendelea kutangaza,

**Inaendelea uk...7**

# VITA YA IRANI NA ISRAEL HATARI ZAKE KWA UMMA NA HUKUM YA KISHERIA JUU YAKE

Umma wa Kiislamu unashauku kubwa ya kumpata shujaa atakayewafuta machozi yanayo wabubujika tangu kuanguka kwa Khilafah mwaka 1924 Miladi, bali hata kabla ya kuanguka rasmi Umma ulikuwa na machozi kwa dhulma ulizofanyiwa na hao waangushaji wa Khilafah

Baadhi ya Waislamu katika Umma wamefikia kiwango cha kutaka kukata tamaa kwamba Umma hauna tena nusra wala ushindi dhidi ya maadui wa Uislamu.

Na kwa hakika Muislamu kufikia kiwango hicho ni jambo hatari kubwa katika aqida kwani ni kupingana na Quran Tukufu inayothibitsha ushindi na nusra kwa Umma huu wa Kiislamu

Kwa miaka ya hivi karibuni Umma wa Kiislamu uliwahi kuweka matarajio yao kwa Saddam Huseni lakini hana alichokifanya, zaidi ya kukamatwa ndani ya shimo akiwa mchafu chakari dhooful-hali na mali na hatimaye akanyongwa kidhalili kabisa.

Pia Umma ukaweka matarajio ya kwa Gadafi, debe tupu lenye kuvuma lisio na kitu ndani. Naye akaishia kukamatwa kwenye mitaro ya maji machafu na kuburuzwa jangwani kama mzoga wa punda na kufa kifo cha mateso, dhalili na cha fedheha

Umma ukahamishia matarajio yao kwa Iran. Na hakuna shaka Iran ameshaubwaga Umma wa Kiislamu kitambo.



Kitu kibaya sana katika nafsi za Umma wa Kiislamu kuona kwamba Allah Taala katutelekeza na hatupi tena nusra , au kudhani leo hii hakuna tena Waislamu wachamungu wenye kustahiki kupewa nusra na Allah Taala.

Muislamu kuwa na fikra za hayo mawili ni ushindi wa wazi kwa makafiri maadui wa Waislamu, Uislamu na ubinadamu

Kinachowapa ushindi makafiri leo ni kwamba wanapigana vita bandia na vibaraka wao, ambapo vibaraka hao wanafanya michezo ya kuigiza, katika hali kama hiyo makafiri hawajapata mpinzani wa kweli na wakapambana nae.

Mfano Iran; badala ya kupiga Israel mpaka kuifanya majivu, ilikuwa inasubiri ipigwe kwanza, ndio na wao wapige. Hii ni wazi Iran haina shida wala dhamira ya kupigana kutaka kumshidna adui.

Lakini cha ajabu zaidi ni pale ambapo Iran inataoa taarifa kwanza kabla ya kushambulia ili kumjuulisha adui atatumia silaha aina gani, athari za silaha, muda na eneo.

Kwa maigizo haya ni wazi Iran haina nia ya dhati ya kupigana na Israel.

Hivyo, chochote kitakachotokea kwa Iran basi Umma usivunjike moyo. Kwani Iran inaweza kuuza misimamo yake na kupigwa na kuvurugwa na isifanye lolote licha ya silaha nzito alizonazo.

Iran haitekelezi vigezo na masharti ya Kiislamu, hivyo kushindwa ni jambo la kutarajiwa.
Amma hukmu ya kisheria juu ya vita hivi ni kama ifuatavyo:

**1.** Madam yahudi adui bado amekalia ardhi za Kiislamu basi hukmu ni apigwe mpaka atoke au kubakie jivu Tel Aviv na sio mkataba wala makubaliano.

**2. Israel inapaswa** ipigwe kwa kuvamiwa bila taarifa, kwani hiyo ndio hukmu ya mvamizi, tofauti na inavyofanya Iran

**3.** Adui Yahudi apigwe kwa nguvu zote na sio nguvu kidogo au kiasi, tofauti na Irani ambapo anaipiga Israel kwa kugusagusa na kwa kuwapa taarifa za mashambulizi.

**4.** Iran ilikuwa itangaze jihadi dhidi ya Israel kwa Umma ili uitikie wito, na bila shaka Umma wa Kiislamu wote wangesimama na Iran

**5. Uislamu unawajibisha** kutozitambua sheria zinazoitwa za kimataifa,jumuiya zao, mikutano yao na masharti yao. Kwani hao ndio maadui wakubwa wa Uislamu

Amma nusra kwa Umma wa Kiislamu, hili ni swala la muda tu, nusra itarudi na Waislamu watafurahi pale Khilafah Rashida ya pili itakaposimama.

ويومئذ يفرح المؤمنون بنصر الله

*"Na siku hiyo watafurahi Waumini, kwa nusra ya Allah"*

ya AFCON 2027 na kugharamia Uchaguzi Mkuu. Imefafanuliwa kuwa katika bajeti hii malipo ya riba za mikopo ni shilingi trilioni 6.49, ruzuku (subsidies & transfers) kwa taasisi za Serikali, mashirika ya umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa shilingi trilioni 22.17 na shilingi trilioni 7.72 zitatumika kugharamia malipo ya mtaji kwa deni la ndani na nje.

Vipaumbele hivi vya serikali ni aibu kubwa na matusi kwa masikini ambao wanahangaika usiku na mchana kujaribu kupata japo mkate wa siku bila mafanikio. Pesa nyingi zitatumika katika mambo yasiyo na maana yeyote kwa watu kama vile kuimarisha miundombinu ya michezo na hasa mpira wa miguu kwa ajili ya mashindano ya AFCON 2027. Kwa watu ambao hawajui watakula nini, ni kiwango cha ukatili kiasi gani hiki kupelekwa fedha za Umma katika mambo ya anasa na starehe badala ya kutatua mahitaji msingi ya binadamu?

Hii ni kwa kifupi kuhusu matumizi ya bajeti hii. Kwa upande wa vyanzo vya mapato, bajeti inatarajiwa kugharamiwa na mapato ya ndani ya shilingi trilioni 40.47, misaada shilingi trilioni 1.07 na mikopo ya shilingi trilioni 14.95. Kati ya mapato ya ndani yanayotarajiwa, mapato ya kodi ni shilingi trilioni 32.31, mapato yasiyo ya kodi shilingi trilioni 6.48, na mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa shilingi trilioni 1.68. Aidha, mikopo inajumuisha shilingi trilioni 6.27 kutoka vyanzo vya ndani na shilingi trilioni 8.68 kutoka vyanzo vya nje.

Bajeti inatoa matarajio hewa kwa wananchi katika upande wa mapato na kufanya ongezeko la bajeti lisilo na maana yeyote.

Katika bajeti iliyopita 2024/2025 ilikuwa shilingi trilioni 50.29 kutoka katika vyanzo vya ndani na nje. Hadi Mei 2025, serikali inadai ilikuwa imekusanya kiasi cha shilingi trilioni 45.07 kati ya pesa hizo mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ambayo ndiyo chanzo kikuu cha mapato ya serikali yalikuwa shilingi trilioni 26.86 pekee.

Mapato yasiyo ya kodi yanayokusanywa na Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali, yalikuwa shilingi trilioni 2.97, na mapato yaliyokusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa yalifikia trilioni 1.26, sehemu iliyobaki ya hiyo trilioni 45.07 iliyokusanywa mwaka 2024/2025 ni mikopo na misaada.

Kwa taswira hiyo, inaonesha wazi kuwa uwezo wa mapato ya kindani ni shilingo takribani trilioni 30 pekee na kuweka bajeti kubwa ya trilioni 50.29 kama ilivyokuwa mwaka jana au trilioni 56.49 kama ilivyo mwaka huu ni kudanganya watu na kudhihirisha utegemezi kwa mataifa na mashirika ya kikoloni.

Utegemezi huu unajidhihirisha wazi kupitia kukua kwa deni la taifa na kufikia shilingi trilioni 107.7 trilioni kutoka Shilingi trilioni 91.7 mwaka jana. Hii inamaanisha serikali imekopa shilingi trilioni 16 ndani ya mwaka mmoja! Pesa hizi zitalipwa kwa riba na bila shaka zitaongeza mzigo mkubwa wa kodi kwa masikini.

Haya yote yanadhihirisha machoni kwetu mambo kadhaa ikiwemo kushindwa kwa ubepari na demokrasia yake katika kusimamia watu, ukoloni na unyonyaji wa rasilimali za mataifa machanga unaofanywa na mataifa ya kikoloni unaopelekea utegemezi wa kudumu wa mataifa machanga kwa mataifa na mashirika ya kikoloni.

Ni muda muafaka sasa kwa ulimwengu kuangalia mfumo mwingine utakaoweza kuunusuru uchumi, ulimwengu, bajeti za mataifa machanga na kuondoa umasikini.

Mfumo huo ni Uislamu chini ya Dola yake tukufu ya Khilafah ambayo itatekeleza sera za uchumi wa Kiislamu na kuondoa kodi za dhulma (tax/maks), kuzuiya riba, kupambana na unyonyaji na kuweka usawa na uadilifu katika kunufaika na mali za Ummah.

********

## BAADHI YA MATUKIO YA MUHARRAM

**1.Mwaka Mpya wa Kiislamu.**

Kuanza Mwaka Mpya wa Kiislamu.

**2.Kuangamizwa Fir-aun na Kuokolewa Nabii Mussa. (A.S)**

Allah alimnusuru Mussa A.s kwa kumuokoa na kuangamizwa Firaun.

**3.Kuangamizwa Abraha na Majeshi yake baada ya Kutaka Kuivunja Al-kaaba.**

(Tarehe 17 Muharram siku kama 50 kabla ya kuzaliwa SAAW. Mwaka wa 571 AD)

"Vivyo hivyo, tutakuwa na AMANI, hivi karibuni, kati ya Israel na Iran! Miito mingi na mikutano inafanyika sasa." (Sky News, 15/6/2025)! Tunatahadharisha dhidi ya vita hivi kuleta amani na umbile la Kiyahudi, bali, kama Mwenyezi Mungu alivyosema:

[فَإِمَّا تَثْقَفَنَّهُمْ فِي الْحَرْبِ فَشَرِّدْ بِهِمْ مَنْ خَلْفَهُمْ]

**"Basi ukiwakuta vitani wakimbize walio nyuma yao ili wapate kukumbuka."** [Al-Anfal:57].

4- Lakini kinachovunja moyo kweli ni watawala Ruwaibidha (wajinga wasio na maana) katika nchi za Waislamu, hususan zile zinazolizunguka umbile la Kiyahudi linaloikalia kimabavu Palestina. Wanawazunguka, basi iweje wasione ndege za Kiyahudi zikipita juu ya vichwa vyao, zikipiga mabomu nchi za Kiislamu na kurudi salama bila hata risasi moja kufyatuliwa?! Badala yake, wao kana kwamba ni watu wasioegemea upande wowote wanaotazama yanayoendelea, kana kwamba wako katika nchi fulani ya mbali, si katika ardhi za Waislamu! Watawala hawa wako katika hali ya kuangamia na hilo halishangazi, kwani wako kwenye mvuto na wito wa nchi za kikoloni za makafiri hususan Amerika. Wanasema wanachosema na kufanya wanachotaka. Wanahalalisha kutochukua hatua na kutukuza mipaka, na wakasahau au wanajifanya kusahau kuwa ardhi za Waislamu ni moja, sawa iwe ziko katika sehemu ya mbali zaidi ya dunia au iliyo karibu zaidi! Na kwamba amani ya Waumini ni moja, na vita vyao ni vimoja. Sio sawa zigawanyike kwa madhehebu yao ya Kiislamu, maadamu wao ni Waislamu, kwani wao ni Ummah mmoja:

[إِنَّ هَذِهِ أُمَّتُكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً وَأَنَا رَبُّكُمْ فَاعْبُدُونِ]

**"Kwa hakika huu umma wenu ni umma mmoja, na Mimi ni Mola wenu Mlezi. Kwa hivyo niabuduni Mimi."** [Al-Anbya: 92].

Iweje ndege za adui ziruke juu ya anga ya watawala katika nchi za Waislamu na kuipiga mabomu nchi nyingine ya Kiislamu huku wao wakinyamaza kimya?! Mfano zaidi wa haya ni njia ya wale wanaotazama ndege za adui zikija na kuondoka kana kwamba haziegemei upande wowote au wako karibu na Mayahudi! Aidha, ijapokuwa watawala hawa wanasikia kauli ya Trump, sio vidokezo vyake, kwamba umbile la Kiyahudi linapigana kwa kamba (msaada) ya Amerika, amri zake, na silaha zake, lakini hakuna hata mmoja wao anayesubutu angalau kukata mahusiano na Amerika.

[أَلَا سَاءَ مَا يَحْكُمُونَ]

**"Tazama uovu wa wanavyohukumu!"** [An-Nahl: 59]

5- Pamoja na hayo yote, Ruwaibidha (watawala wasio na maana) hawa watatoweka na Dola ya Kiislamu, Khilafah Rashida, itaregea kuwa dola ya kwanza duniani, ikieneza kheri ndani yake, Mwenyezi Mungu akipenda. Kupigana na Mayahudi na kuondoa uvamizi wao kutatokea, Mwenyezi Mungu akipenda. Mkweli na Mwaminifu (saw) amesema katika Musnad Ahmad kutoka kwa Hudhayfah:

«ثُمَّ تَكُونُ خِلَافَةً عَلَى مِنْهَاجِ النُّبُوَّةِ...»

**"...kisha kutakuwa na Khilafah kwa njia ya Utume."**

Kadhalika, Al-Bukhari amepokea kutoka kwa Abdullah ibn Umar, Mwenyezi Mungu awe radhi nao wote wawili, ambaye amesema: Nimemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) akisema: « تُقَاتِلُكُمُ الْيَهُودُ فَتُسَلَّطُونَ عَلَيْهِمْ..» **"Mayahudi watapigana nanyi. Basi mtawadhibiti juu yao"** Imepokewa pia na Muslim kutoka kwa Ibn Umar, kutoka kwa Mtume (saw) ambaye amesema: « لَتُقَاتِلُنَّ الْيَهُودَ فَلَتَقْتُلُنَّهُمْ..» **"Kwa yakini mtapigana na Mayahudi, na mutawaua."** Kisha dunia itang'aa kwa ushindi wa Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

[إِنَّ فِي ذَلِكَ لَذِكْرَى لِمَنْ كَانَ لَهُ قَلْبٌ أَوْ أَلْقَى السَّمْعَ وَهُوَ شَهِيدٌ]

**"Hakika katika hayo upo ukumbusho kwa mwenye moyo au akatega sikio naye yupo anashuhudia."** [Qaf: 37]

Kwa kumalizia, Hizb ut Tahrir, kiongozi asiyewadanganya watu wake, inakuombeni muiunge mkono na mufanye kazi nayo kuiregesha Khilafah Rashida kwa mara nyengine tena, ili Uislamu na watu wake uheshimiwe na ukafiri na watu wake wadhalilike, na huo ndio utakuwa ushindi mkubwa.

[وَيَوْمَئِذٍ يَفْرَحُ الْمُؤْمِنُونَ * بِنَصْرِ اللَّهِ يَنْصُرُ مَنْ يَشَاءُ وَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ]

**"Na siku hiyo Waumini watafurahi. Kwa nusura ya Mwenyezi Mungu humnusuru amtakaye. Naye ndiye Mwenye nguvu Mwenye kurehemu."** [Ar-Rum: 4-5]

# HIZB UT TAHRIR TANZANIA YAZINDUA KAMPENI MAALUM YA KULINDA NA KUTETEA AQIDA YA KIISLAMU

**Taarifa Kwa Vyombo Vya Habari**

Mnamo tarehe 2 Muharram 27 Juni 2025 Hizb ut Tahrir Tanzania mara baada ya Swala ya Ijumaa ilizindua kampeni maalumu ya kitaifa katika Masjid Rahma Buguruni, jijini Dar es Salaam.

Dhamira ya kampeni hiyo ya muda wa miezi miwili ya Hijria (Muharram 1447- Swaffar 1447 Hijria ni kuilinda na kuitetea Aqeeda ya Kiislamu.

Mnamo tarehe 2 Muharram 27 Juni 2025 Hizb ut Tahrir Tanzania mara baada ya Swala ya Ijumaa ilizindua kampeni maalumu ya kitaifa katika Masjid Rahma Buguruni, jijini Dar es Salaam.

Dhamira ya kampeni hiyo ya Kampeni hii imekuja kufuatia kuenea, kuchipuka harakati za kipotofu ambazo hueneza muda wa miezi miwili ya Hijria (Muharram 1447- Swaffar 1447 Hijria ni kuilinda na kuitetea Aqeeda ya Kiislamu fikra mbali nyuma ya pazia ni kupambana na Uislamu na kutia shaka Waislamu na dini yao.

Kampeni hii ina malengo yafuatayo:

Kugonga Fikra ya Dini Mseto
Kugonga Fikra ya Upagani
Kubomoa Aqeeda ya Dini za Jadi na dini za uafrika
Kumakinisha Ufahamu Sahihi wa Aqeeda ya Kiislamu kwa upana wake.

Kampeni hii imebeba Kauli Mbiu ya: *"Kataa Dini Mseto, Ukristo, Upagani, Mizimu, baki na Uislamu"*

Kampeni itatumia mbinu mbali katika kujitangaza, kufikisha ujumbe wake kwa Umma kama:

Majukwaa ya wazi ya Kiislamu
Mihadhara ya wazi na Wakristo na makundi yote mengine yanayobeba fikra dhidi ya Uislamu.
Uandishi na utawanyaji wa makala mbali kwa Umma na katika mitandao ya kijamii Kuandika na kufikisha nyaraka kwa taasisi na jumuiya mbali zisizo za Kiislamu kuonesha udhaifu wa fikra zao na kufafanua ukweli wa Uislamu
Kutawanya vidio fupifupi katika mitandao ya kijamii.
Kutumia majukwaa ya Khutba za Ijumaa
Kutoa taarifa kwa vyombo vya habari
Kufanya amali za kutangaza kwa mabango(picketing)
Kufanya vipindi katika Tv za mitandao, redio nk.

Hizb ut Tahrir Tanzania inatoa mwito kwa wanajamii kushiriki kikamilifu katika kampeni hiyo. Kwa Waislamu kupata ufafanuzi ziada kwa dini yao. Na wasiokuwa Waislamu watapata fursa adhimu kuutafiti Uislamu kwa hoja na dalili za kiakili.

Masoud Msellem

Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari Hizb ut Tahrir Tanzania

Kumb: 1447/01 Ijumaa 02 Muharram 1447 H/ 27 Juni 2025 M

**#DiniYaHakiUislamuTu**




**Masoud Msellem**

Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari Hizb ut Tahrir Tanzania alipokuwa akizindua Kampeni yenye kaulimbiu "**Kataa dini mesto, Ukristi, upagani, mizimu, bakia na uislamu**" baada ya swala ya ijumaa